

Jinsia haizidi nyingine, wote ni sawa

"Togbé" ni mkuu wa familia isiyo masikini kabisa. Ana uwezo wakujibu mahitaji ya familia yake. Mtu huyu ni mkulima mkubwa, anayejulikana kwa kijiji kizima kama "Djègbadji". Hahimizi elimu ya wasichana hata kidogo na anapendezwa zaidi na wavulana kwa sababu tofauti. Kwa mtu huyu, kumpeleka msichana shuleni ni kama kutupa pesa zake nje ya dirisha au ni kama kumwaga maji mgongoni mwa bata. Kwa yeye, wasichana shuleni mara nyingi hupata ujauzito na mwishowe hukua pamoja na waume zake. Ambayo labda ni chanzo cha taka kwa mtu huyu.

Akiwa na familia ya watoto wanane wakiwemo wavulana watano na wasichana watatu, Togbé, kila wakati katika filozofia yake, aliweza kupeleka wanawe shule na kupendekeza kwamba wasichana wabakie nyumbani kwa kazi ya nyumbani hadi, atakapoamua kuwatafutia wachumba.

Agossi, msichana mdogo zaidi akikua, mara nyingi hufadhaika sana wakati anaona dada zake wakubwa wakifanya kazi nyumbani kila siku. Agossi hakukubali kuishi katika hali hiyo kama dada zake, aliamua kwa matumaini, kuwaacha wazazi wake na kujiunga na familia ya mjomba wake wa mama katika kijiji kingine cha karibu.

Huko, kufikia matarajio yake, mjomba wake " Bossou " alimsajili katika shule ya umma kutoka kijiji hicho kipya. Tayari kwa Agossi lengo lake limefikiwa kutoka siku ya kwanza ya usajili wake. Alifurahi sana, alikuwa mwanafunzi na mjanja sana, ambaye kila mtu alipenda shuleni. Baada ya shule ya msingi na shule ya upili, alipata udhamini na alitumia miaka mitatu katika mafunzo ya chuo kikuu katika uandishi wa habari, ambapo baadaye alishinda kazi katika kituo cha redio cha mkoa jijini.

Leo kijiji chake chote, wazazi wake, husikia sauti yake kupitia matangazo anayowasilisha, na amekuwa msichana wa mfano kutoka mkoa wote. Kuita kipindi fulani cha matangazo ya redio juu ya "kusoma watoto" siku moja, aliishia kuhitimisha na yafuatayo: " **Jinsia haizidi nyingine, wote ni sawa** ".

Anaandika Bernard Gnancadja

Imetafsiriwa na Joel Muhire na Elisee Byelongo ambaye ameichunguza kilugha, tarehe 24 novemba 2021.